**Hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, wakati Akizindua Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Viwango Tanzania (Tanzania Bureau of Standards – TBS)**

---

**Dar es Salaam, (Ofisi za TBS), Alhamisi 08 Julai 2021**

---

Ndugu Dotto James, Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara
Dkt. Yusufu Athuman Ngenya, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS)
Wakurugenzi na Wakuu wa Idara mbalimbali za Wizara ya Viwanda na Biashara
Wakuu wa Taasisi Mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara
Wakurugenzi na Wakuu wa Idara na Watumishi wengine wa TBS
**Mabibi na Mabwana!**

***Ninawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!! Kazi Iendelee!!***

Ninashukuru kwa fursa hii ya kuzungumza katika hafla hii muhimu ya kuzindua Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Viwango nchini (Tanzania Bureau of Statistics-TBS). Sitaki kudanganya na kusema kwamba ninawashukuru kwa kunialika na kunipa heshima ya kuwa mgeni rasmi. Ukweli ni kwamba mie ndiye niliyeagizi hafla hii iandaliwe leo kwa ajili ya kuzindua rasmi Bodi hii ambayo tumeiteua hivi karibuni. Nilifanya hivi kwa kuwa nilitaka muanze kazi mara moja.

Ninawapongeze wajumbe wote kwa uteuzi mlioupata. Hongera Mwenyekiti, Dkt. Fenella Mukangara, na wajumbe wote kwa uteuzi wenu. Hongera sana Dkt. Fenella kwa heshima ambayo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amekupatia kwa kukuteua kuwa Mwenyekiti wa Bodi na wajumbe wote kwa heshima ambayo Mheshimiwa Waziri amewapa kwa kuwateua kuwa wajumbe wa Bodi. Tunawapongeza sio tu kwa uteuzi mlioupata, lakini pia kwa heshima mliyoipata ya kutumikia Shirika la Viwango nchini (TBS), ambalo ni moja ya mashirika ya umma bora na yanayoheshimika nchini na katika ukanda wa Afrika. Tunaamini kwamba nyie ambao

mmepata heshima hii ya uteuzi mtalinda heshima na hadhi ya TBS ili liendelea kuwa shirika bora daima.

Katika kuwateua nyie kuwa wajumbe tumezingatia kikamilifu matakwa ya sheria husika. Zaidi, tumezingatia sifa za msingi ambazo wajumbe wa Bodi wa Shirika la Umma kama hili wanapaswa kuwa nazo. Sifa hizi ni pamoja na ***maadili*** (integrity), ***uwezo wa kuelewa mambo, uwezo wa kufanya kazi katika timu,*** na ***uwezo wa kuwakilisha maslahi mapana ya wadau/wabia*** wa Shirika la Viwango Tanzania. Tumezingatia sifa mchanganyiko za wajumbe ili ndani ya vikao kuwe na mijadala yenye afya, ikiwemo uwezo wa kutofautiana kimtazamo bila kupoteza urafiki, ushirikiano na hali ya utimu miongoni mwa wajumbe. Muhimu kabisa tumechagua wajumbe ambao tunaamini watajiamini na kufanya kazi zao bila hofu wala woga na kwamba watakuwa na uwezo wa kuwa na uhusiano chanya na wenye afya na wadau wakubwa wa TBS bila kuathiri uwezo wao wa kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Tunaweza kufafanua neno "kiwango" kama njia ambayo jamii imekubaliana kufanya jambo fulani kwa aina fulani. Kiwango kinaweza kutumika katika maeneo mbalimbali, ikiwemo bidhaa, huduma, mifumo, n.k. Uwepo wa viwango ndiyo huhakikisha uwepo wa usalama, afya na ubora katika jamii.

Hapa Tanzania Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ndilo lililokabidhiwa mamlaka ya kutengeneza na kusimammia utekelezaji wa viwango. Katika majukumu yake TBS inaongozwa na Sheria ya Viwango Tanzania ya Mwaka 2009. Sheria hii inaainisha majukumu 20 ya Shirika. Baadhi ya majukumu haya ni: kusaidia viwanda kuweka na kusimamia utekelezaji wa mifumo ya ubora; kutoa elimu kuhusu viwango; kukusanya, kuchapisha na kusambaza taarifa kuhusu viwango; na kupima ubora wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi kabla hazijasafirishwa. Jukumu kubwa la Bodi ambayo tunaizindua leo itakuwa ni kusimamia menejimenti ili itekeleze majukumu haya.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Kisheria na kimuundo, Shirika la TBS linaendeshwa kwa utatu: ***Serikali, Bodi*** na ***Menejimenti***. Moja ya eneo muhimu la kueleweka mapema ni majukumu ya Bodi, majukumu ya Menejimenti na majukumu ya Serikali/Wizara. Hili ni suala ambalo lina

mjadala mpana sana katika nadharia ya Bodi za mashirika ya umma na hata ya binafsi. Hivyo, ningetaka tutumie fursa hii kuelewana mapema sana kuhusu majukumu haya ili tuepuke uwezekano wowote wa mgongano wa maslahi na mgongano wa majukumu miongoni mwa wahusika, kwa maana ya serikali, Bodi na Menejimenti.

Kimsingi jukumu kuu la serikali ni mmiliki wa shirika na hivyo wajibu wake wa msingi ni kutoa sera na malengo mapana ya shirika, pamoja na usimamizi wa jumla wa shirika. Kwa ufupi, serikali inatoa matokeo tarajiwa ya shirika. Jukumu la msingi la Bodi ni kutengeneza mkakati wa kufikia malengo ya shirika na kusimamia utekelezaji wake, ikiwemo kutoa mpango wa upimaji wa matokeo. Jukumu la msingi la Menejimenti ni kutekeleza mkakati wa kufikia malengo ya shirika na kuwajibika kwa kufikiwa au kutokofikiwa kwa malengo tarajiwa.

Ukisoma sheria, na ukizingatia nadharia ya majukumu ya Bodi, unayaona majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi katika maeneo matatu makubwa. Mosi, jukumu la Bodi linaonekana katika kutoa ushauri na unasihi ndani na nje ya vikao vya Bodi. Ushauri ni katika maeneo mengi yenye tija kwa Shirika, ikiwemo, kwa mfano, utatuzi wa changamoto zinazozijitokeza; mawazo mapya ya kuboresha uendeshaji wa shirika; huduma mpya ambazo shirika linaweza kuanzisha katika kuimarisha utendaji na hadhi yake; kutatua migogoro inayoweza kujitokeza miongoni mwa watumishi; na kukosoa mwenendo wa shirika. Ili wajumbe waweze kutekeleza jukumu hili ni sharti wawe na uelewa mpana kuhusu shirika, jamii na mwelekeo wa kisera wa serikali na nchi kwa ujumla.

Pili, Bodi inatarajiwa kuwa mtunza nidhamu wa Mkurugenzi Mkuu na Menejimenti ya Shirika kwa niaba ya mmiliki wa Shirika (Serikali). Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa Menejimenti inatekeleza majukumu ya msingi ya Shirika na kuhakikisha kuwa Shirika linaendeshwa kwa mujibu wa Sheria, kanuni na taratibu zilizopo, na kwamba Bodi inawajibika kuhakikisha wakati wote maslahi ya mwenye Shirika yanazingatiwa kikamilifu. Ili kutekeleza jukumu hili kikamifu inatarajiwa ***Bodi itatengeneza na kusimamia viwango na vigezo vya kupima utendaji wa Menejimenti*** ambayo matumizi yake yameidhinishwa na mwenye Shirika na kwamba viwango na vigezo hizi mara zote vitazingatia Sheria na Kanuni za utumishi za umma.

Tatu, Bodi inatarajiwa kutoa au kushiriki kutoa utatuzi wakati Shirika linakabiliwa na changamoto za kimenejimenti. Hii ni pamoja na kuwa na ujasiri wa

kutoa ushauri, wenye kuzingatia ushahidi usio na shaka, wa kubadilisha menejimenti pale ambapo ni wazi kuwa Menejimenti haitekelezi majukumu yake ipasavyo. Ufanisi katika kutekeleza jukumu hili unategemea uwepo wa viwango na vigezo vya wazi vya kupima utendaji wa Menejimenti. Aidha, Bodi inatarajiwa iwe juu ya majanga yote yanayoweza kulikumba Shirika ili Bodi iendelee kuwa na maana machoni mwa watumishi, umma na mwenye Shirika.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Katika muktadha niliyoueleza hapo juu, hatima ya shirika ipo mikononi mwa Bodi inayofanya kazi kwa niaba ya serikali. Kawaida, serikali itatekeleza majukumu yake kupitia kwa Bodi ya Wakurugenzi. Hivyo, kama Bodi itatekeleza majukumu yake ipasavyo, hakuna sababu ya msingi ya Serikali kuingilia kati utendaji wa Shirika kwa njia ya matamko na maelekezo. Hata hivyo, ni wazi kuwa Bodi sio muamuzi wa mwisho wa hatima ya Shirika, bali ni mshiriki na mshirika muhimu sana wa michakato ya maamuzi kuhusu Shirika. Washiriki wengine muhimu katika maamuzi ya Shirika ni Serikali (Mmiliki) na Menejimenti (mwenye jukumu la kuendesha *affairs* za kila za shirika).

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Kuna mambo machache ya kuzingatia katika kuhakikisha panakuwepo na mahusiano chanya na yenye tija kati ya Bodi, Menejimenti na Serikali. Ninaendelea kusisitiza kwamba vyombo hivi vitatu vitahitajiana na lazima vifanye kazi kama timu mara zote katika kuhakikisha kuwa Shirika linakwenda vizuri na linatekeleza majukumu yake ipasavyo. Kiungo muhimu katika Timu hii ni Mkurugenzi Mkuu na Menejimenti yake. Baadhi ya mambo ya kuzingatia ili kila moja wetu atekeleze majukumu yake ni haya yafuatayo:

i) ***Uelewa kuhusu Shirika***: Hatua ya kwanza ni kwa wajumbe kuelewa vizuri maana, malengo, na majukumu ya Shirika, pamoja na sheria na kanuni zinazoendesha Shirika. Hii pia inahusu wajumbe kuelewa muktadha na kiachoendelea dunia kuhusu sayansi ya viwango na mashirika ya viwango duniani. Moja ya chanzo cha migogoro kati ya Menejimenti na Bodi na/au

Bodi kuwa tu mtia muhuri wa maamuzi ya Menejimenti ni uelewa mdogo wa wajumbe kuhusu mambo wanayoyasimamia

ii) ***Falsafa ya utendaji wa Bodi***: Zipo falsafa mbili zinaweza kutumiwa na Bodi katika kuendesha Shirika. Baadhi ya wataalam wa Menejimenti ya mashirikia wameita falsafa hizi kama Usheria vs. Kuongeza tija/thamani (***Conformance versus performance***): Katika hali ya kawaida, Bodi inafanya kazi kupitia Menejimenti ya Shirika. Hivyo, vitu vingi vitakavyoletwa katika Bodi vitaletwa na Menejimenti baada ya kufanyiwa kazi na wataalam na vitalazimika kuletwa katika Bodi kwa kuwa Sheria na taratibu zinataka hivyo. Ni juu ya Bodi na nyie wajumbe kuamua falsafa yenu ya utendaji: kwamba mtaamua kutekeleza majukumu yenu tu ya msingi ya kisheria na kikanuni kwa kuwa Sheria inataka Bodi iwepo au mtataka muongeze thamani katika Shirika. Ni jukumu la wajumbe kutambua kuwa jukumu lao sio tu kuwepo hapa kwa mujibu wa sheria, bali kutambua kuwa wanahitajika kuongeza tija na thamani katika Shirika hili. Tunatarajia muisaidie Menejimenti katika kutatua changamoto za msingi na katika kuhakikisha kuwa TBS inaendelea kuwa Shirika bora linalokidhi matakwa ya jamii na ambalo nchi inajivunia na kwamba linakuwa Shirika lenye hadhi stahiki kikanda na kidunia. Kufanya hivi kutawalazima nyie wajumbe kusaka taarifa na maarifa ya ziada zaidi ya kile mtakacholetewa mezani. Ni kwa sababu hii tumeteua wajumbe wenye sifa mchanganyiko sana kwa kuzingatia weledi wao na historia yao nzuri ya kiutendaji na mwenendo wa kitabia.

iii) ***Kuwa na viwango na vigezo vya kupima utendaji wa Menejimenti***: Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa Bodi inavitumia vigezo hivyo na kutokuona aibu wala woga katika kupima utendaji wa Mkurugenzi Mkuu na timu yake ya Menejimenti

iv) ***Bodi kuelewa majukumu yake sawa sawa na wajumbe kujiepusha na kufanya kazi za Menejimenti***: Moja ya changamoto inayokabili bodi nyingi za mashirika ni wajumbe kutoelewa majukumu yao au kujisahau na kujikuta wanaingilia majukumu ya Menejimenti. Ni muhumi Mwenyekiti na wajumbe wakajitambua mapema kwamba wao sio waajiriwa wa Shirika la Viwango Tanzania. Hivyo, wajumbe wasije wakajikuta wanaanza

kulitegemea Shirika katika kuendesha maisha yao ya kila siku au katika kutatua changamoto zao za kifamilia na kijamii. Pale wajumbe wakijikuta wanaanza kujihusisha na utendaji wa kila siku wa Shirika watajikuta wanaanza kuwa kero kwa Shirika badala ya kuwa msaada. Kujiingiza katika majukumu ya Menejimenti pia kutawanyima wajumbe fursa ya kujadili mambo ya kimkakati na kulielekeza Shirika ipasavyo.

v) ***Ushirikiano, kuthaminiani, kusikilizana na upendo:*** Kwa kiasi kikubwa mafanikio yenu yatategemeana sana uhusiano mwema na hali ya utimu (team work) mtakayojenga miongoni mwenu. Hivyo, niwakumbushe kudumisha ushirikiano, kuthaminiana, kusikiliza na mara kupendana kama familia moja ya TBS.

Ninapohitimisha hotuba yangu, ninaomba niwakabidhi mambo matatu ili Bodi yenu iyashughulikie, ikiwezekana katika kikao chenu cha kwanza. Mosi, ni suala la TBS kufanya kazi ya kuweka vinasaba. Serikali ilishafanya uamuzi wa msingi kwamba TBS wafanye kazi hii na tayari TBS wanaifanya kazi hii. Hata hivyo, taarifa ya tathmini iliyofanywa na EWURA inaonesha kuwa kuna maeneo ambayo bado TBS hawafanyi vizuri. Bodi ikaipitie taarifa hiyo na kuhakikisha kuwa maeneo yote kuhusu kazi hii yanakaa sawa.

Pili, serikali pia ilifanya uamuzi wa kuanza kufanya ukaguzi wa magari yanayoagizwa kutoka nje hapa hapa nchini. Kazi hii pia wamekabidhiwa TBS na tayari walishaanza kuifanya. Hata hivyo, kumeibuka malalamiko mengi kutoka kwa wadau. Baadhi ya malalamiko haya nimemkabidhi Mwenyekiti wa Bodi. Bodi ikae na kuyafanyia kazi malalamiko haya mapema. Kazi hii lazima ifanyika kwa ufanisi ili nchi yetu isije kugeuka kuwa mahala pa kutupikia magari yaliyomalizika muda wake kutoka nje.

Tatu, ni kuhusu wafanyabishara ndogo na wenye viwanda vidogo. Wengi wa hawa wamekuwa wakilalamika kutokutambuliwa bidhaa zao na TBS na kwamba TBS hawawapi ushirikiano wa kutosha. Ni vizuri niwakumbushe kuwa serikali imeweka mkazo mkubwa sana kwa kundi hili kwa kuwa lina nafasi nzuri sana ya kuzalisha ajira. Hivyo wafanyabishara ndogo na wenye viwanda vidogo ni muhimu wakasaidiwa. Aidha, TBS ina nafasi nzuri sana ya kusaidia jitihada za serikali katika kurasimisha

biashara za kundi hili. Hivyo, Bodi itengeneze mkakati wa kuharakisha utambuzi wa biashara na uzalishaji wa kundi hili haraka iwezekanavyo.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Ninawatakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yenu. Ni imani yetu kuwa katika kipindi chenu TBS itaendelea kuwa shirika bora na kung'ra zaidi kitaifa, kikanda na kimataifa. Sasa ninayo furaha kutamka kuwa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Viwanda Tanzania (TBS) imezinduliwa rasmi leo hii siku ya Alhamisi tarehe 08 Julai, 2021.

**Mungu Awabariki!**